www.tvla.go.tz

# TVLA HABARI

ISO/IEC 17025:2017
ACCREDITED

Toleo la 001 Mei -Oktoba 2024

# MIAKA MITATU

## ya Utendaji Kazi wa Rais Samia

**NDANI**

**Ifahamu Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA)**

**Taarifa ya Wakala kuhusu utekelezaji wa shughuli za maendeleo katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**



# KUTOKA MEZA YA MTENDAJI MKUU



Karibu katika usomaji wa ***Jarida la TVLA HABARI***, jarida hili linatolewa kila baada ya miezi sita likiwa na habari, picha, makala na taarifa mbalimbali zinazohusu Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA).

Lengo kuu la jarida hili ni kuelimisha umma juu ya mambo mbalimbali yanayofanywa na Wakala.

Katika toleo hili la kwanza tumelenga kutoa taarifa ya utekelezaji wa shughuli za maendeleo za Wakala kwa kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Jarida hili pamoja na kuchapishwa pia litakuwa likipatikana katika tovuti ya Wakala na kurasa zetu za mitandao ya kijamii, hivyo kutoa fursa na nafasi kubwa kwa kila msomaji kuwa na ufahamu na kuelimika juu ya majukumu mbalimbali yanayotekelezwa na Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA).

Mpendwa msomaji nachukua nafasi hii kukukaribisha kwa moyo mkunjufu, kufuatilia na kusoma jarida hili na matoleo mengine yajayo. Asante.

**Mtendaji Mkuu wa Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA) Dkt. Stella Bitanyi**

## MAWASILIANO

Majengo ya Veterinari,
131 Barabara ya Nelson Mandela,
S.L.P 9254, Dar es Salaam.
Simu +255 22 2861152,
Nukushi +255 22 2864369,
Barua pepe: info@tvla.go.tz,
Tovuti: www.tvla.go.tz

## 1. UTANGULIZI

Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA) ni Wakala ya Serikali iliyo chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, iliyoanzishwa kwa Sheria ya Wakala za Serikali Na. 245 (iliyofanyiwa marekebisho Mwaka 2009) na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali la tarehe 9 Machi 2012. Wakala hii ilizinduliwa rasmi tarehe 11 Julai, 2012.

Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania ilitokana na kuunganishwa kwa iliyokuwa Maabara Kuu ya Mifugo (CVL), Vituo vya Kanda vya Uchunguzi na Utambuzi wa Magonjwa ya Mifugo (VICs), Taasisi ya Utafiti wa Ndorobo (TTRI) Tanga na Kituo cha Utafiti wa Ndorobo (TTRC) Kigoma.

### 1.1 DIRA YA WAKALA

Dira kuu ya Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania ni kuwa kituo cha umahiri katika kutoa huduma bora za uchunguzi wa kimaabara, bidhaa bora za Veterinari na kufanya utafiti wa magonjwa ya wanyama na wadudu waenezao magonjwa hayo ndani na nje ya Tanzania.

### 1.2 DHAMIRA YA WAKALA

Dhamira ya Wakala ni kutoa mchango stahiki katika kuimarisha uzalishaji endelevu wa Sekta ya Mifugo, usalama wa chakula na kuchangia kwenye uchumi wa taifa kupitia utoaji wa huduma bora za uchunguzi na utambuzi wa magonjwa ya mifugo kwa gharama nafuu, uzalishaji na usambazaji wa bidhaa bora za veterinari na kufanya tafiti za magonjwa ya wanyama na wadudu waenezao magonjwa hayo.

## 2. MAJUKUMU YA WAKALA

Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA) inatekeleza majukumu mahususi kulingana na malengo ya kuundwa kwake ambayo ni pamoja na;

1) Uchunguzi na utambuzi wa magonjwa ya wanyama
2) Uzalishaji na usambazaji wa chanjo za mifugo
3) Uhakiki wa ubora wa vyakula vya mifugo
4) Usajili na uthibiti wa ubora wa viuatilifu vya mifugo
5) Utafiti wa magonjwa ya wanyama na wadudu waenezao magonjwa hayo
6) Kutoa huduma za ushauri na mafunzo

## 3. AINA ZA CHANJO ZINAZOZALISHWA NA WAKALA

Wakala inazalisha chanjo aina saba (7) na wastani wa uzalishaji kwa mwaka ni dozi milioni 65 ambazo huzalishwa kwa kuzingatia mahitaji ya soko. Uwezo kamili wa uzalishaji wa chanjo kwa sasa ni zaidi ya dozi milioni 100 kwa mwaka.
Wakala kupitia mikakati iliyonayo ya shughuli ya uzalishaji na uuzaji wa chanjo inatarajia kuzalisha kwa wingi chanjo hizo ili kukidhi soko la ndani na nje ya nchi.

Chanjo zinazozalishwa na Wakala ni pamoja na:-

i) Chanjo stahimilivu joto ya kukinga kuku dhidi ya Ugonjwa wa Mdondo;
(ii) Chanjo ya Ugonjwa wa Kimeta;

(iii) Chanjo ya Ugonjwa wa Chambavu;
(iv) Chanjo ya Homa ya Mapafu ya Ng'ombe;
(v) Chanjo ya Ugonjwa wa Kutupa Mimba;
(vi) Chanjo mchanganyiko wa Kimeta na Chambavu; na
(vii) Chanjo ya Homa ya Mapafu ya Mbuzi.




## 4. VITUO VYA WAKALA

Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania inatekeleza majukumu yake kupitia vituo mbalimbali vilivyopo katika Kanda nchi nzima. Pamoja na Vituo hivyo pia kuna Vituo viwili vya Wakala ambavyo ni Maabara Kuu ya Mifugo (Central Veterinary Laboratory, CVL) na Kituo cha Magonjwa Ambukizwa na Bioteknolojia (Centre for Infectious Diseases and Biotechnology – CIDB) vilivyoko Temeke, Dar es Salaam. Vituo hivi viwili ni Maabara za rufaa za wanyama ambazo hupokea sampuli kutoka maabara za Kanda na kufanya uchunguzi na utambuzi kwa kutumia vipimo vyenye uwezo zaidi na vina wataalamu wabobezi katika nyanja mbalimbali tofauti na vipimo vinavyofanywa na maabara za Kanda.

**Vituo 11 vya kikanda ambavyo hutoa huduma zitolewazo na Wakala nchini ni:**

(i) Taasisi ya Chanjo Tanzania (TVI) - KIBAHA-PWANI ambayo kazi yake pekee ni kufanya tafiti za chanjo na kuzalisha chanjo za mifugo.
(ii) Maabara ya Veterinari Kanda ya Kati - DODOMA
(iii) Maabara ya Veterinari Kanda ya Nyanda za Juu Kusini – IRINGA
(iv) Maabara ya Veterinari Kanda ya Ziwa - MWANZA
(v) Maabara ya Veterinari Kanda ya Kaskazini - ARUSHA
(vi) Maabara ya Veterinari Kanda ya Magharibi - TABORA
(vii) Maabara ya Veterinari Kanda ya Kusini – MTWARA
(viii) Maabara ya Kanda ya Kusini Magharibi-SUMBAWANGA, Rukwa
(ix) Maabara ya Kanda ya Ziwa Magharibi MEATU, SIMIYU.
(x) Kituo cha utafiti wa magonjwa yaenezwayo na wadudu kwenye wanyama– VVBD – KIGOMA
(xi) Kituo cha utafiti wa magonjwa yaenezwayo na wadudu kwenye wanyama- VVBD- TANGA.



# TAARIFA YA MTENDAJI MKUU KUHUSU UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA MAENDELEO ZA WAKALA KATIKA KIPINDI CHA MIAKA MITATU YA UONGOZI WA MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania-TVLA ni Wakala iliyo chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi yenye Dira kuu ya kuwa Kituo cha umahiri katika kutoa huduma bora za Maabara za Veterinari, bidhaa bora za Veterinari na kufanya utafiti juu ya magonjwa ya wanyama na wadudu waenezao magonjwa hayo ndani na nje ya Tanzania.

Dhamira yetu Kuu ni kuimarisha uzalishaji endelevu wa sekta ya Mifugo, Usalama wa Chakula na kuchangia kwenye uchumi wa Taifa kupitia utoaji wa huduma bora za uchunguzi na utambuzi wa Magonjwa ya wanyama kwa gharama nafuu, huduma bora za uchambuzi wa kiveterinari, uzalishaji na usambazaji wa bidhaa bora za veterinari na kufanya tafiti juu ya magonjwa ya wanyama na wadudu waenezao magonjwa hayo.

Ili kuweza kufikia malengo hayo Wakala imekabidhiwa majukumu makuu 6 ambayo ni: -

1. Kufanya uchunguzi na utambuzi wa Magonjwa ya Wanyama;
2. Kuzalisha na kusambaza chanjo za mifugo;
3. Kufanya uhakiki wa ubora wa vyakula vya mifugo;
4. Kusajili na kuthibiti ubora wa viuatilifu vya Mifugo;
5. Kufanya tafiti zinazolenga kupata njia za kudhibiti/kutokomeza magonjwa ya Wanyama na wadudu waenezao magonjwa hayo; na
6. Kutoa huduma za ushauri na mafunzo.








*Uhakiki wa ubora wa vyakula vya mifugo*

Wakala katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Mhe.Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wakala inajivunia mafanikio mbalimbali iliyoyapata katika kutoa huduma na kuzalisha bidhaa za kiveterinari hapa nchini.



Miongoni mwa mafanikio hayo ni pamoja na: -

1. Kuongeza kiwango cha ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Wakala kutoka Shilingi bilioni 2.5 mwaka 2021 hadi kufikia shilingi bilioni 3.2 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 28. Ongezeko hili la mapato lilisaidia kuimarisha na kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Wakala kikamilifu, kuendelea kupunguza utegemezi Serikalini na kuendelea kuchangia kwenye mfuko mkuu wa Serikali.

2. Kupatikana kwa ithibati (accreditation) ya vipimo vya Maabara katika uchunguzi na utambuzi wa magonjwa ya wanyama kulingana na kanuni za uchunguzi wa kimaabara unaokubalika kimataifa. Hatua hii imeifanya nchi kutolazimika kupeleka sampuli nje ya nchi kwa lengo la kuthibitisha matokeo ya ugonjwa yaliyotolewa na maabara za ndani ya nchi, lakini pia kukubalika kwa matokea ya maabara zetu kimataifa.



Cheti cha Ithibati



SADCAS
SOUTHERN AFRICAN DEVELOPMENT COMMUNITY ACCREDITATION SERVICE

CERTIFICATE OF ACCREDITATION

TANZANIA VETERINARY LABORATORY AGENCY
*Established under Executive Agencies Act, CAP 245*

**Facility Accreditation Number:** VET 007

is a SADCAS accredited Testing Laboratory
provided that all SADCAS conditions are complied with

This certificate is valid as per the scope stated in the accompanying schedule of accreditation, Annexure "A", bearing the above accreditation number for

**PATHOLOGY, MOLECULAR BIOLOGY and SEROLOGY**

*The facility is accredited in accordance with the recognized International Standard*

**ISO/IEC 17025:2017**

*The accreditation demonstrates technical competency for a defined scope and the operation of a laboratory quality management system*

*SADCAS is a subsidiary organization of SADC. A memorandum of understanding between SADC and SADCAS serves as the basis for the recognition of SADCAS by SADC Member States as a multi-economy accreditation body*

Mrs Maureen P Mutasa
SADCAS Chief Executive Officer

Effective Date (Issue No: 1): 25 March 2022
Certificate Expires: 24 March 2027

3. Kupandisha hadhi kliniki ya Meatu iliyopo Mkoa wa Simiyu na kuwa kituo kamili cha Wakala chenye kuhudumia kanda ya Ziwa -Mashariki.

4. Ukamilishaji wa ujenzi wa jengo la Maabara kwa ajili ya uzalishaji wa chanjo za magonjwa ya Wanyama yatokanayo na bakteria uliogharimu Shilingi Milioni 778.

Ujenzi huo ulienda sambamba na ununuzi wa vifaa na mashine za maabara zilizosimikwa kwenye Taasisi ya Chanjo Tanzania na Maabara Kuu ya Veterinari – Temeke (DSM) ambavyo viligharimu kiasi cha Shilingi bilioni 3.6



*Kituo cha TVLA Meatu-Simiyu*



*Jengo la Maabara ya uzalishaji wa chanjo za magonjwa ya Wanyama yatokanayo na bakteria*

5. Kujenga jengo jipya la kituo cha TVLA Iringa, ambapo awali kituo kilikuwa kikitumia jengo dogo lisilokidhi mahitaji ya wafugaji wa Kanda ya Nyanda za juu Kusini. Ujenzi wa jengo hilo la kisasa la Ofisi na Maabara uligharimu kiasi cha Shilingi Milioni 307 hadi kukamilika kwake.


Jengo jipya la kituo cha TVLA Iringa

6. Wakala katika kipindi hicho cha miaka mitatu ilinunua magari nane (8) yaliyogharimu kiasi cha shilingi Bilioni 1.068. Awali Wakala ilikuwa na changamoto kubwa ya kukosa vyombo vya usafiri kwenye vituo vyake na hivyo kushindwa kutoa huduma kwa ufanisi kwa wananchi. Ununuzi wa magari hayo umepunguza changamoto ya usafiri kwa kiasi kikubwa na hivyo kuboresha utoaji wa huduma.



7. Kukarabati miundombinu ya maabara na ofisi za vituo vya Tabora, Sumbawanga, Mtwara, Arusha na Maabara Kuu ya Veterinari


Jengo lililoboreshwa TVLA Mtwara


Jengo lililoboreshwa-TVLA Arusha



Pia Wakala imeweza kufanya ukarabati wa nyumba tatu wanazoishi watumishi na hivyo kuendelea kuboresha mazingira ya ufanyaji kazi kwa Watumishi. Katika uboreshaji huo kiasi cha Shilingi milioni 60 kilitumika.



*Nyumba ya mtumishi wa TVLA-Tanga kabla ya ukarabati*



*Nyumba ya mtumishi wa TVLA-Tanga baada ya ukarabati*



*Baadhi ya watumishi wa TVLA*

8. Kuongezeka kwa uzalishaji wa chanjo za mifugo kutoka aina sita (6) hadi kufikia chanjo aina saba (7). Aidha, kiwango cha uzalishaji kimeweza kupanda kutoka dozi milioni 48 zilizokuwa zikizalishwa mwaka 2021 hadi kufikia dozi milioni 65 mwaka 2024 ambapo kwa miaka mitatu Chanjo zilizozalishwa ni dozi milioni 198.3.

Huu ni ukombozi mkubwa kwa wafugaji hapa nchini kwani kwa wale wanaozingatia utoaji wa chanjo kulingana na maelekezo wamefanikiwa kudhibiti magonjwa ya mifugo kwa kiwango kikubwa.




***Chanjo iliyoongezeka ya Homa ya Mapafu ya Mbuzi (CCPP)***

Mfano matumizi ya Chanjo inayokinga kuku dhidi ya Ugonjwa wa Mdondo yamepunguza vifo vilivyokuwa vikitokana na ugonjwa huu kwa zaidi ya asilimia 95 kwenye maeneo mengi hapa nchini ikiwemo mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

9. Kuanza hatua za utengenezaji wa Chanjo za Magonjwa ya Kichaa cha Mbwa na Sotoka ya Mbuzi na Kondoo ambazo utengenezaji wake upo katika hatua mbalimbali na majaribio.

10. Kuboresha miundombinu ya Maabara kuu ya Veterinari iliyopo Temeke –Dar es salaam kwa kufanya ununuzi wa vifaa vya kisasa ambapo kiasi cha shilingi milioni 320 zimetumika kwenye uboreshaji huo.

Uboreshaji wa miundombinu umewezesha uhakiki wa sampuli za vyakula 6,115. Aidha, uboreshaji wa miundombinu kwa kununua mashine za kisasa za maabara umewezesha wateja kupata majibu ya sampuli zao kwa baadhi ya vipimo ndani ya sikumojahivyokupunguzamudawakusubiri.

11. Kufanikiwa kupata fedha za ufadhili katika miradi mbalimbali zaidi ya shilingi bilioni 3.2 ambazo zilitumika katika kufanya tafiti zilizowezesha upatikanaji wa vifaa vya kimaabara, kujengea uwezo wataalamu wa maabara katika uchunguzi na utambuzi wa vimelea vya magonjwa na upatikanaji wa mbinu za kudhibiti magonjwa ya wanyama na binadamu pamoja na wadudu wanaoyaeneza.

Kwa mfano Kupitia tafiti za kuangamiza Mbung'o wanaoeneza ugonjwa wa Nagana kwa ng'ombe na Malale kwa binadamu, teknolojia mbalimbali zimeibuliwa ikiwa ni pamoja na matumizi ya mitego ya vitambaa inayonasa Mbung'o pamoja na teknolojia ya vifukuzi na vivutizi.
Vifukuzi ni kemikali zinazotoa harufu ya Kuro ambaye hang'atwi na Mbung'o hivyo vikifungwa kwenye shingo ya ng'ombe, mbung'o hawasogei. Vivutizi ni aina ya kemikali ambayo huwekwa kwenye mitego na kuwavutia Mbung'o na wakishaingia hawawezi kutoka.


Mitego ya kuangamiza mbung'o


Maabara Kuu ya Veterinari



12. Aidha, Katika kipindi cha miaka hii mitatu Wakala iliweza kupata jukumu jipya la kuhakiki na kudhibiti ubora wa viuatilifu vya mifugo pamoja na kusajili. Jukumu hili limeanza kutekelezwa kuanzia mwezi Julai 2022. Serikali imeendelea kuboresha maabara inayotumika kuwezesha jukumu hili kufanyika kwa ubora na viwango vya kimataifa.

Hadi kufikia Machi, 2024 imetoa vibali vya kuingiza viuatilifu (import permits) 110, imesajili viuatilifu viwili (2), imehuisha usajili *(Registration renewal)* wa viuatilifu kumi na tano (15), ambapo vitatu (3) vinatumika kuzalishia viuatilifu (Technical material) na (12) ni vya viuatilifu vinavyotumika moja kwa moja kuua wadudu kwenye wanyama, imehuisha vibali vinne (4) vya kufungasha viuatilifu *(Repackaging Certificate)*, imeuhisha kibali kimoja cha kuzalisha viuatilifu nchini *(Formulator Certificate),* imehuisha vibali 81 vya kuuza viuatilifu vya wanyama kwa jumla na rejareja (Wholesale/Retail selling permits) pamoja na kuhuisha vibali 37 vya waagizaji wa viuatilifu nchini *(Importer's certificates).*





13. Katika kipindi cha miaka mitatu pia Wakala imeweza kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali kwa kutoa shilingi milioni 180 hivyo kusaidia katika kuwezesha Serikali kuendelea kutoa huduma kwa wananchi.

14. Sambamba na utoaji wa Gawio kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali, Wakala ilifanikiwa kusaidia jamii mbalimbali zenye uhitaji hasa makundi maalumu kama walemavu na wahitaji wengine pamoja na Taasisi mbalimbali ikiwa ni sehemu ya urudishaji kwa jamii (CSR) kwa kile ilichofanikiwa kuzalisha ambapo jumla ya misaada yenye thamani ya Shilingi milioni 105 ilitolewa.

15. Katika kuendelea kuimarisha utekelezaji wa majukumu, Wakala inaishukuru Serikali chini ya Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuboresha maslahi, stahiki na Mishahara ya watumishi (Kuongezeka kwa viwango vya posho mbalimbali kwa watumishi, kuongezwa kwa mishahara) jambo ambalo limeendelea kuleta morali ya ufanyaji wa kazi na hivyo kuongeza tija.

Aidha mazingira ya utendaji kazi kwa Watumishi yameendelea kuboreka kwa kuongeza upatikanaji wa vitendea kazi kwa watumishi (Ununuzi wa Kompyuta, vifaa vya ofisi, samani na vitendea kazi vya maabara) 16.

Kuongezeka kwa idadi ya watumishi wa kada mbalimbali kutoka watumishi 182 hadi kufikia 192 na hivyo kupelekea pengo la Watumishi wanaoihitajika kupungua kwa kiasi kikubwa.





## VITUO VYA WAKALA YA MAABARA YA VETERINARI TANZANIA (TVLA)

Wakala ina vituo kadhaa vilivyopo sehemu mbalimbali nchini ambavyo ni; Makao Makuu Temeke- Dar es salaam, Maabara Kuu ya Mifugo (CVL) iliyopo Temeke, Kituo cha uchunguzi wa Magonjwa ya kuambukiza na Bioteknolojia (CIDB)-Temeke, Taasisi ya chanjo Tanzania (TVI) iliyopo Kibaha Mkoa wa Pwani.

Pia Wakala ina mitandao ya Maabara kote nchini ambazo ni; Arusha, Dodoma, Iringa, Mtwara, Meatu-Simiyu, Mwanza, Tabora na Rukwa- Sumbawanga. Pia tuna Vituo viwili vya Utafiti wa Magonjwa yaenezwayo na wadudu vilivyopo Tanga na Kigoma.

### NAMBA ZA KUPIGA SIMU BURE KWA VITUO VYOTE VYA WAKALA YA MAABARA YA VETERINARI TANZANIA (TVLA) VINAVYOTOA HUDUMA NCHINI

| NA | MIKOA (VITUO) | NAMBA ZA KUPIGA SIMU BURE |
|---|---|---|
| 1 | DAR ES SALAAM - HQ | 0800750275 |
| 2 | DAR ES SALAAM - CIDB | 0800750276 |
| 3 | DODOMA | 0800750277 |
| 4 | MWANZA | 0800750278 |
| 5 | ARUSHA | 0800750279 |
| 6 | TANGA | 0800750280 |
| 7 | IRINGA | 0800750281 |
| 8 | TABORA | 0800750282 |
| 9 | MEATU - SIMIYU | 0800750283 |
| 10 | SUMBAWANGA - RUKWA | 0800750284 |
| 11 | KIGOMA | 0800750285 |
| 12 | MTWARA | 0800750286 |

Majengo ya Veterinari, 131 Barabara ya Nelson Mandela, S.L.P 9254, Dar es Salaam. Simu +255 22 2861152,
Nukushi +255 22 2864369, Barua pepe: info@tvla.go.tz, Tovuti: www.tvla.go.tz

## MWISHO

Wakala inamshukuru Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kutenga bajeti kila mwaka kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu na huduma za Wakala.

Sisi kama Wakala tunampongeza kwa uongozi wake makini na dhamira ya dhati aliyonayo katika kuhakikisha shughuli za ufugaji nchini zinakuwa na tija na hivyo kuongeza mchango kwenye pato la taifa na kuinua uchumi wa wananchi.

Pia tunaendele kuwakaribisha wananchi kutumia huduma zetu zinazopatikana katika vituo vyetu.



www.tvla.go.tz

# TVLA HABARI

ISO/IEC 17025:2017 ACCREDITED

*Mtendaji Mkuu wa Wakala ya Maabara ya Veterinari nchini (TVLA) Dkt. Stella Bitanyi akisisitiza jambo wakati akifungua Mafunzo ya Wazalishaji na Wasambazaji wa vyakula vya Mifugo mikoa ya Pwani na Dar-es-salaam Disemba 20, 2023. Kulia kwake ni Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Uendelezaji Malisho na Rasilimali za vyakula vya Mifugo Bw. Rogers Shengoto na Kulia kwake ni Mkurugenzi wa Huduma na Uchunguzi wa Wakala hiyo Dkt. Zacharia Makondo.*





*Muuzaji wa vyakula vya Mifugo kutoka Wilaya ya Kibaha mkoani Pwani Bi. Domitela Melisa (Kulia) akitoa ushauri kuhusu lishe ya kuku kwa mmoja wa wafugaji aliyefika dukani kwake (kushoto) Wanaoshuhudia katikati ni Meneja wa Maabara Kuu ya Veterinari nchini Dkt. Geofrey Omarch na Mkaguzi wa vyakula vya Mifugo kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi Bi. Theodata Salema waliofika dukani hapo kukakagua namna huduma ya vyakula vya Mifugo inavyotolewa.*



*Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipango, Masoko na Habari kutoka Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA) Bw. Prosper Haule akikabidhi Chanjo ya Mdondo wa Kuku aina ya TEMEVAC kwa Bi. Alice Tenga Muuzaji wa duka la pembejeo za Mifugo (Temboni VET) lililopo Goba jijini Dar es Salaam Oktoba 10, 2023 alipofanya ziara ya kutembelea maduka yanayouza bidhaa za TVLA*



*Meneja wa Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania-TVLA Kanda ya Kati Dodoma Dkt. Japhet Nkangaga (mwenye miwani) akitoa elimu kwa wadau wa Mifugo waliotembelea banda la TVLA kujifunza kazi zinazofanywa na TVLA pamoja matumizi sahihi ya Chanjo za Mifugo zinazozalishwa na TVLA kwenye Maonesho ya pili ya Kilimo ni Biashara Kilimo katika Mbio za Marathon 2023 yaliyofanyika Gairo Morogoro*